**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA**
**SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO**

**Namba za simu** **S.L.P 324,**
**Mkuu wa Shule 0765783530** **KYELA.**
**Makamu Mkuu wa Shule 0682419034** **18/04/2024**
**Matron 0757559947**

---

MZAZI/ MLEZI WA MWANAFUNZI ……………………… … S. L. P ……………

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAFUNDO HALMASHAURI YA KYELA, MKOA WA MBEYA, MWAKA 2024</u>**

**1.0** Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano (**V)** katika shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya HGK / HGL. Shule ya Sekondari KAFUNDO ipo umbali wa kilomita 20 kutoka kyela mjini. Usafiri wa basi kutoka Kyela mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Kyela Mjini, nauli ni Tsh. 1,500/= tu hadi Ipinda Mjini. Kutoka Ipinda mjini anaweza kutembea kwa miguu au akatumia pikipiki (Bodaboda) kwa Tsh 1,000/= hadi shule ya sekondari Kafundo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 01/07/2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024 .Mwisho wa kuripoti ni tarehe 07/07/2024.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### SARE YA SHULE.

(i) Sketi mbili rangi ya **dark blue (blue nyeusi)** na **kijivu** kitambaa kizito. Mshono uwe rinda pana mbele na nyuma, ziwe ndefu sana (Ziguse viatu). Kitambaa kimeambatanishwa, tafadhali zingatia rangi na aina ya kitambaa.)

(ii) Mashati mawili meupe tetroni mikono mirefu yasiyobana au yasiwe mafupi

(iii) Viatu vya ngozi, rangi nyeusi jozi mbili, vyenye kamba na visivyo na visigino virefu.

(iv) Soksi rangi nyeupe jozi mbili.

(v) Tai rangi inayoendana na sketi

(vi) Sweta mbili moja rangi ya kijivu na nyingine blue nyeusi (dark blue) (vii) Tracksuit rangi ya bluu bahari(Light blue) (viii) Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo.

(ix) T-shirt inapatikana shuleni

(x) Gauni la kazi (Out of school uniform) rangi ya bluu bahari (light blue) ndefu isiyobana. (Nguo za nyumbani haziruhusiwi)

(xi) Kwa Waislamu hijabu nyeupe zisizokuwa na urembo.

**3. MICHANGO YA SHULE.**

a) Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi/mlezi mara mwanafunzi anaporipoti shuleni: -

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**MUHIMU:** ***Michango yote ni Tsh 80,000/= ilipwe kwenye akaunti ya shule. Tafadhali andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi kwenye pay in slip na kuwasilisha siku ya kuripoti shuleni.***

JINA LA AKAUNTI**:** **KAFUNDO SECONDARY SCHOOL**
NAMBA YA AKAUNTI**:** **60901200036 NMB**

**4. MAHITAJI MUHIMU MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI.**

**(a) Mahitaji ya mwanafunzi**.

i. Mashuka mawili rangi ya bluu bahari (light blue)
ii. Chandarua
iii. Blanketi dogo au shuka zito kwa ajili ya baridi
iv. Nguo za ndani za kutosha na mahitaji muhimu ya wasichana
v. Taulo moja, kanga au kitenge
vi. Nguo ya kulalia (Night dress) moja
vii. Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
viii. Godoro linakodishwa shuleni kwa gharama ya **shilingi 10,000/=** kwa mwaka,(italipwa shuleni ).

**(b) Mahitaji ya Taaluma na vifaa vya usafi wa mazingira.**

(i) Bunda mbili za karatasi kwa mwaka(Ream A4)
(ii) Daftari kubwa 8 (Counter books Quire 3)

(iii) Kalamu za wino na risasi
(iv) Mkebe wenye vifaa na Rula
(v) Vitabu vya masomo ya tahasusi yake orodha imeambatanishwa.
(vi) Flat file moja (spring file)
(vii) Ndoo mbili, moja lita ishirini na ndogo ya lita kumi zenye mifuniko
(viii) Brash ngumu 1, mopa 1, ufagio wa ndani mmoja (soft bloom) na wa nje mmoja (chelewa) .
(ix) Jembe 1 lenye mpini, kwanja 1 na Reki 1.

**5.1 Sheria na kanuni muhimu za shule .**

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoligia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.Mambo hayo ni pamoja na ;

(i). Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote,wanafunzi wengine, na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
(iii) Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (preparation );
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa ;
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo utakayopewa;
(vi) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya shule;
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
(ix) Kutunza mali za shule;
(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari;
(xi) Mwanafunz harusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.**
- **Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake aukuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa.**
- **Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.( Msiba au Ugonjwa)**

**5.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na** i. Wizi;

ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji sigara;
ix. Uasherati ,mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule; xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**J.Nombo**
**JENNY.A.NOMBO**
**MKUU WA SHULE.**

**NB: Kwa siku za hivi kaaribuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao).**
**Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni wanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE ,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATZO;**

- **Mkuu wa shule 0765783530**
- **Makamu mkuu wa shule 0682419034**
- **Mwandamizi Taaluma 0768163526/0625755266**
- **Mwandamizi Malezi 0757559947.**

**7. Viambatisho na fomu muhimu**

i. Fomu zote muhimu zilizoambatanishwa zijazwe kikamilifu na kwa usahihi ; ii. mwanafunzi aje na picha nne (4 ) za wazazi na ndugu wa karibu wa wanafunzi.

**MKUU WA SHULE**

# FOMU A

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**
**(THIS FORM IS TO BE COMPLETED BY A MEDICAL OFFICER).**

Name of pupil ………………………………………………………………………………………….

Age ………………………………………………… Sex …………………………………………..

The above named has been examined in respect of

(a) STOOL ……………………………………………………………………………

(b) URINE ……………………………………………………………………………..

(c) CHEST …………………………………………………………………………….

(d) BLOOD …………………………………………………………………………….

(e) EYES ………………………………………………………………………………

(f) EARS ……………………………………………………………………………….

(g) OTHER FINDINGS …………………………………………………………....

…………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………….………………………………

…………………………………………………………………………………….....................

I am satisfied that the above named pupil is /is not fit to pursue further studies in any secondary school.

………………………………….. ………………………………

SIGNATURE DATE

…………………………………. ……………………………..

DESIGNATION STATION

# FOMU B

## FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

**(IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)**

Mimi (taja jina lako kamili) ……………………………………………………………. nimechaguliwa kujiunga na masomo ya Elimu ya Sekondari kidato cha tano **(V) 2024** katika Shule ya Sekondari Kafundo. Najaza fomu hii kukubali kuchaguliwa kwangu kuendelea na masomo katika shule hii. Naahidi kuwa niwapo katika shule hii nitatii na kufuata sheria na kanuni zote za shule kwa kipindi chote cha masomo yangu.

Pia naahidi kuwa, kwa muda wote ni wapo katika shule hii sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Kama nitakiuka na kwenda tofauti na mkataba huu, naomba sheria kali zichukuliwe dhidi yangu yaani **kufukuzwa shuleni** na **kushtakiwa Mahakamani**.

Nakubali kuwa nimesoma na kuelewa yote katika fomu hii ya mkataba na ninaahidi kuwa nitatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule.

**SAHIHI YA MWANAFUNZI** ……………………………

**TAREHE** ……………..……………………………………

# FOMU C

## FOMU YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI, KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE.

**(IJAZWE NA MZAZI / MLEZI MWENYEWE)**

Mimi mzazi / mlezi (Jina kamili ……………………………………………….……………. ambaye ni mzazi / mlezi wa (Jina kamili la mwanafunzi) ………………………………………………. najaza fomu hii kukubali maelezo yaliyoandikwa hapo juu. Kwa kujaza fomu hii, naahidi kuwa nitatekeleza kwa vitendo katika kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapata mahitaji yote (yake binafsi na mahitaji ya shule) kwa muda wake wote wa masomo ya Elimu ya Sekondari akiwa Kafundo Sekondari.

Iwapo sitatimiza wajibu wangu, naahidi kuwa sheria zichukuliwe dhidi yangu.

**SAHIHI YA MZAZI / MLEZI** ………………………………..…….

**TAREHE** ………………………………………………………...…

# FOMU D

## HABARI KUHUSU MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi (Jina hili ndilo litakalotumika siku zote bila kubadilika)

…………………………………………………………………………………………………….

2. Tarehe ya kuzaliwa: …………………………………………...……………………………

3. Mahali alipozaliwa (Wilaya): ………………………………...……………………………….

4. Mahali anapoishi sasa (Wilaya): ……………………………………………………………..

5. Jina la Baba / Mlezi: ……………………………………………………………………….

6. Anuani ya Baba /Mlezi ……………………..……………………………………………

7. Jina la Mama / Mlezi: ……………………………………………………………………

8. Dini ya Mwanafunzi: ……………………………………………………………………

9. Dini ya Baba / Mlezi: ……………………………………..……………

10. Dini ya Mama / Mlezi: ……………………………………………………………………..

11. Kazi ya Baba / Mlezi: ……………………………………...…………………………….

12. Namba ya simu ya mzazi/mlezi………………………………………………………………..

13. Michezo atakayoshiriki shuleni ni: ………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………..

## RANGI YA KITAMBAA CHA KIJIVU

KIJIVU MPAUKO(GRAYSCALE)